

KESI

 Baba yetu aliye Mbinguni, tunakushukuru kwa majaliwa tuliyo nayo ya kukusanyika chini ya dari hii alasiri ya leo, tena, kusikiliza Neno la Mungu, na kuona utukufu wa Bwana Yesu Kristo. Tuko kwenye matarajio makuu, Baba. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utatupokea alasiri ya leo, na kujali jitihada zetu tunazotoa kuja kukuabudu Wewe. Bariki kila nafsi iliyo hapa. Tunatambua ya kwamba mambo mazuri ni yale ambayo ni magumu kuyapata. Kwa hiyo tunaomba, ya kwamba kwa sababu ya kujitolea kwao, hakutakuwa na mtu ye yote aliyesalia ila yule atakayeponywa alasiri ya leo. Waokoe waliopotea na ujiipatie utukufu Wewe Mwenyewe. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mwaweza kuketi.

² Paa letu la bati kwa namna fulani linafanya hali kuwa ngumu kwenu kusikia. Hatutachukua ila wakati mfupi tu, kuzungumza nanyi. Na halafu basi tutaendelea moja kwa moja na mstari wa maombi, maana hayo ndiyo tuliyoupangia alasiri ya leo, ilikuwa ni kuwaombea wagonjwa.

³ Na sasa nataka kusema jambo hili. Sijui kama nimewahi kufurahi kuwa na kundi la watu wakati wowote zaidi ya nilivyofurahi kuwa na kundi hili hapa. Mmekuwa wazuri kweli. Nilikuwa nikimwambia Ndugu Johnson, muda mfupi uliopita, ya kwamba sijui ni lini nilipopata kufurahia kukutana na watu walio wazuri kuliko hawa. Roho nzuri sana kati yenu enyi watu, na jinsi mnavyoamini, imani yenu. Ningependa kukaa hapa kama mwezi mmoja, kusudi tupate kuzoeana kabisa sisi kwa sisi. Kwa kawaida, inapokaribia wakati wa kuzoeana, basi ndipo wakati mtu inapokulazimu kusema “kwa heri” na kwenda sehemu zingine.

⁴ Sijui maskini huyu polisi aliyepo hapa nje ni nani, anayesimama pale nje kwenye mvua yote hiyo, bila kofia, akishughulika na kuelekeza magari. Endapo mtu yeyote anamfahamu, mpeni shukrani zangu binafsi nawaomba, sivyo? Nakwambia, yeye amefanya kazi nzuri sana.

⁵ Ninataka kumshukuru mtu aliyekuwa hapa na kupasafisha mahali hapa, na kupatengeneza kwa ajili ya jambo hili, kusudi mkutano huu upate kuwa hapa leo. Ninawaambia, jamii inawiwa shukrani kuu kwa watu wenye maazimio wa jinsi hii, ambao watafanya mambo hayo. Ninawawia shukrani kuu, kwa watu watakaokuja kwenye siku kama hii. Watu wengi wangekaa nyumbani. Ni—ninafurahia ushujaa wenu. Na ninyi mnaosimama hapa katikati ya shida hizi zote, mkiketi chini ya dari hii, ambapo ni vigumu kusikia yanayoendelea, bali

hata hivyo mmeyakinia kukaa kwa vyovyote. Huo ni, huo ndio ushujaa wenyewe. Na—napenda jambo hilo. Daima mimi huwazia juu ya ule wimbo:

Je! yanibidi kubebwa nyumbani Mbinguni
Katika kitanda kizuri cha starehe,
Wakati wengine walipigana wapate kushinda
tuzo,
Na wakaabiri katika bahari za damu? (Naam,
shida!)

⁶ Nilihubiri, wakati mmoja si muda mrefu uliopita, huko Afrika Kusini, ambapo kulikuwa kunanyesha mvua sana katika majira ya pepo za monsuni, mpaka wanawake, wakiwa tu wamekaa kila mahali na nywele zao zikining'inia chini, ikiwa walikuwa wameketi pale siku nzima katika mvua hiyo. Sijawahi kuona mkutano kama huo wa uponyaji maishani mwangu!

⁷ Huko Mexico, si muda mrefu uliopita, ninakumbuka nikiwa nimesimama pale nikihubiri, wakati ilikuwa ikinyesha namna hii, huko nje kwenye uwanja wa mchezo wa ng'ombe kule, siku nzima. Na hao watu walikuwa kule tangu saa tatu asubuhi hiyo, wameketi kwenye mvua. Na mwanamke mmoja akiwa ameshika mtoto aliyekufa mikononi mwake. Mtoto huyo alikuwa amekufa usiku uliopita, maskini mtoto huyo mchanga akiwa amefunikwa amekauka, mikononi mwake. Mtu mmoja alikuwa amesambaza kadi za maombi, na ikawa alikwisha kuzigawa zote. Hakukubaki tena kadi za maombi. Walinishusha kwa kamba, huko nyuma ya uwanja huo, nipate kuingia uwanjani namna hii. Ndipo Billy akanijia mbio. Akasema, “Baba, sijui nitafanya nini.” Akasema, “Nina mabawabu mia tatu waliosimama kule.”

⁸ Na ni wangapi wanaomjua Jack Moore? Karibu ninyi nyote mnamjua Jack Moore, hapa, nadhani. Alikuwa pamoja naye.

⁹ “Na kuna maskini mwanamke mmoja kule nje,” akasema, “aliye na mtoto aliyekufa, alikufa asubuhi ya leo.” Hiyo ilikuwa yapata saa tatu usiku huo. Alikufa asubuhi hiyo katika ofisi ya daktari. Naye akasema, “Anataka mtoto huyo mchanga aliyekufa aletwe mstarini.” Akasema, “Sina kadi zingine tena, na nimekwishawapanga kwenye mstari.” Kasema, “Sijui.” Na mvua Inanyesha kama nini; wamesimama tu pale kwenye hiyo mvua, mvua yenye baridi. Nikaangalia kule nje, na maskini hao wanawake wa Kimexico, nywele zao zikining'inia chini, zimelowa, chepechepe, wakionekana hivyo kwenye mwanga wa hizo taa. Na hungeweza kuona nje, mbele yako, inanyesha sana. Vema, nikasema... “Vema,” akasema, “siwezi kumzuia huyo mama,” kasema, “tuna—tuna mabawabu mia tatu.” Kasema, “Yeye anapanda moja kwa moja juu yao, naye ana mtoto huyu aliyekufa.”

¹⁰ Nikasema, “Vema, Ndugu Moore, kwa nini usishuke uende na kumwomba?” Nami nilikuwa nimehubiri karibu

dakika kumi, nadhani, kitu kama hicho. Ndipo nikasema, “Mbona usiende ukamwombee,” nikasema, “kwa sababu yeye asingenijua mimi, wala mtu yeyote; kumekuwa na wahubiri wengi.” Nikasema, “Yeye hanijui. Wewe nenda ukamwombee mtoto huyo mchanga na hilo litamridhisha.”

¹¹ Akasema, “Vema, Ndugu Branham.” Akaanza kuondoka jukwaani.

¹² Na kulikuwa na lundo la nguo zilizochakaa, lundo namna hii, kote kote kwa urefu, loo, labda wa yadi ishirni ama thelathini. Mwanamume mmoja kipofu alikuwa amefunguka macho, usiku uliotangulia, kwa hiyo walikuwa wamevutiwa kwelikweli. Asilimia tisini ni Wakatoliki.

¹³ Kwa hiyo basi nikaanza kuhubiri. Nikasema, “Kama nilivyokuwa nikisema, imani ni ba- . . .”

¹⁴ Nikaangalia, huyo hapo amesimama mbele zangu, na kulikuwa na maskini mtoto mdogo wa Kimexico, uso mdogo mweusi, fizi ndogo za meno, hana meno, zinang’aa tu, fizi ndogo namna hiyo. Nami nikawazia, “Yule hana budi kuwa ndiye mtoto huyo mchanga.” Nikasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Moore. Mwambie maskini mama huyo mdogo amlete huyo mtoto hapa.”

¹⁵ Kwa hiyo wakafungua, kile chumba, hana—hana kadi ya maombi. Kwa kweli hakupaswa kuingia, bali alikuwa ameng’ang’ania. Hivyo—hivyo ndivyo unavyotaka. Kwa hiyo alikuwa amemleta huyo mtoto mchanga.

¹⁶ Nikasema, “Baba wa Mbinguni!” Kwa kweli, hawafasiri maombi. Nikasema, “Sijui kama huyu ndiye huyo, ama siye. Sasa hivi tu ndiyo nimemwona mtoto huyo mchanga. Lakini kama ndiye, ni heshima Yako kwa mwanamke huyo kwa kujitolea huku.” Nikaweka mikono yangu juu ya hilo blanketi dogo la bluu, na maskini kiwiliwili hicho kidogo baridi kipatacho urefu namna hii, kikiwa kimening’inia katika mikono ya mwanamke huyo.

¹⁷ Ndipo mtoto huyo mchanga akatoa kilio cha nguvu na kuanza kutupatupa miguu, kwa ninii yake yote. . . akilia tu kwa nguvu alivyoweza. Mtoto huyo alikuwa. . . Sasa maskini mama huyo alianguka chini na kuanza kupiga makelele. . . “Padre! *Padre* maana yake ni “baba,” mwajua. Alikuwa ameshika rozari mkononi mwake.

Nikasema, “Hiyo si ya lazima.”

¹⁸ Ndipo nikamwambia Ndugu Espinoza, mhubiri wa Kipentekoste. Wengi, nafikiri, nafikiri mnamjua. Naam, Ndugu Espinoza. Nikasema, “Sasa usiandike, ‘mtoto huyo alikuwa amekufa.’ Sijui mimi. Jambo tu nililoona ni hilo hapo, hilo ono.” Nikasema, “Wewe mfuate m—mtu wa kumkimbilia mwanamke huyo, na aambiwe aende amwambie daktari aandike ripoti juu ya jambo hilo.”

¹⁹ Ndipo gazeti la *Sauti ya Wafanyabiashara* hivi majuzi tu lilandika ripoti hiyo, “Daktari alitoa ushuhuda, ‘mtoto huyo mchanga alikufa akiwa na nimonia maradufu,’ ofisini mwake asubuhi hiyo, ‘saa tatu kasorobo.’” Na wakati huo ilikuwa ni saa nne usiku, Bwana Yesu aliurudisha uhai wake tena, kwa sababu ya kujitolea. Sasa, hiyo ni kweli kabisa! Mungu Mbinguni anajua hiyo ni kweli. Matamshi ya daktari yaliyoidhinishwa! Tamshi hilo sasa limo mikononi mwa Wafanyabiashara Wakristo, ambalo Demos Shakarian ndiye mkurugenzi wa kima-... kimataifa. Yeye ana ripoti iliyotiwa saini na daktari huyo, “Mtoto huyo mchanga alikufa kwa nimonia maradufu, asubuhi hiyo.” Na mnamo saa nne usiku huo mtoto huyo alifufuliwa, kwa sababu ya imani ya mama aliyeng’ang’ana kufanya jambo hilo. Hiyo ni kweli.

²⁰ Ni kama maskini mwanamke yule Mshunami alivyong’ang’ania afike kwa Eliya!

²¹ Ni kama tu vile vile yule mwanamke Myunani Msirofoinike alivyokuwa aking’ang’ania afike kwa Yesu. Alijua alikuwa na binti aliyekuwa na kifafa. Ingawaje, hata hakuwa Myahudi. Uamsho huo haukuwa ni kwa ajili ya watu wake. Na basi wakati Yeye alipofika, wakati mwanamke huyo alipofika Kwake, Yeye alisema, “Haifai kwangu kuchukua chakula cha watoto na kuwapa mbwa.” Alimwita mbwa.

²² Akasema, “Hiyo ni kweli, Bwana.” Angalia jinsi imani halisi itakavyoshuhudia Neno kuwa ni Kweli! “Kweli, Bwana, bali mbwa wako tayari kula mabaki chini ya meza za bwana zao.”

²³ Akasema, “Kwa kusema hivi, mtoto wako ameponywa.” Naye akapata jambo hilo kwa njia ile ile, kwa kuwa alikuwa aking’ang’ania.

²⁴ Asanteni, sana, wapendwa. Bwana na ambariki kila mmoja, wanamuziki, Dada Ungren hapa, na marafiki zangu wote. Ninaona hapa wengi wa marafiki zangu wamekuja kwa ajili ya mkutano huu. Nimewaona, leo, Ndugu na Dada Evans. Sijui kama hata anaweza kunisikia mimi, ama hawezi. Wametoka huko Macon, Georgia. Dada Ungren hapa na—na wote kutoka Memphis, Tennessee. Na Ndugu Palmer na Dada Palmer, na marafiki zao. Na Ndugu Parnell, rafiki yangu mhudumu pale. Ninawaona wameketi tu wamenizunguka kabisa hapa sasa, walio marafiki, marafiki zangu binafsi. Ndugu J.T. hapa, kutoka—kutoka huko Georgia, pia, rafiki yake. Na kwa kweli tunashukuru kuwa na ninyi nyote hapa, na imani yenu na ushujaa wenu. Baadhi ya watu hao wanaendesha magari mpaka Jeffersonville, Indiana, kila Jumapili ninayohubiri huko, wanakuja tu kusikiliza. Ndipo ninawaambia, ya kwamba, ulimwengu hauwastahili watu kama hao, nionavyo mimi. Huyo ni mimi nnayefikiri hayo. Ninyi watu hapa, sisi ni sehemu moja kubwa ya Kristo. Tunamwamni Yeye.

25 Na sasa huu usingekuwa ni mkutano nisipochukua dakika chache kusoma Neno na kutoa matamshi machache. Maana, kama ninyi ni waamnifu vya kutosha kuketi hapa kwa muda huo, mimi ninataka kuwa mwaminifu vya kutosha kwa jambo hilo, kuyasoma Maandiko na kutoa tamshi moja ama mawili, na kisha tutaanza mstari wa maombi.

26 Sasa nitasoma leo kutoka kwenye Maandiko, kutoka Marko mlango wa 16, kwa muda kidogo tu, kutoa somo fulani kutoka kwenye sehemu hii. Nitaanzia kwenye mstari wa 14.

Na baada ya kuwakemea wale kumi na mmoja... akaonekana na wale kumi na mmoja wali... walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.

Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

27 Sasa kumbukeni, “Ulimwenguni mwote, Injili hii, kwa kila kiumbe.” Wengine husema ilikoma kwa mitume. Yeye alisema hapa, ya kwamba, agizo Lake la mwisho kwa Kanisa, lilikuwa, “Ulimwenguni mwote, kwa kila kiumbe. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Wapi? “Ulimwenguni mwote, kwa kila kiumbe.” Angalia, hapo ndipo alipolipa Kanisa hayo; nionyeshe mahali alipoondoa jambo hilo. A-ha. “Ulimwenguni mwote!”

Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini, atahukumiwa.

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya.

Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.

Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.

Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote. Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.

28 Sasa, ninaamni Maandiko hayo kuwa ni Kweli.

29 Kabla sijasahau hilo, mwanangu aliniambia muda mfupi uliopita, maskini bibi mmoja, na mumewe kutoka huko Arkansas, waliniokea keki ya siku ya kuzaliwa na wakanipa. Wengi wenu mmenipa kadi na kadhalika. Hata sijapata nafasi ya kuliongelea jambo hilo bado. Asanteni, sana. Mungu awabariki. Nami ninatumaini ninyi mtakuwa na... sote tutapitisha siku ya kuzaliwa ya Milele huko ng'ambo, ambako tutaketi chini, nami

ninataka ninii—ninataka miaka elfu kumi kukaa pamoja na kila mmoja wenu, tuketi tu chini na kuzungumza. Wala hatutakuwa na wakati wowote uliopunguka, kuzungumza, kuliko tuliokuwa nao tulipoanza. Hiyo ni Kweli. Sasa nawashukuru kwa yote mliyofanya.

³⁰ Sasa kama dakika kumi, ama zisizozidi sana sana kumi na tano, labda, kama Bwana akipenda, kutoa tu maelezo machache.

³¹ Ninataka kusema jambo hili, ya kwamba ninatumaini kwamba jinsi ninavyojisikia, nikiongozwa kuja, ninyi wachungaji mkisikia kuongozwa kunidhamini nipate kuja, hilo linanipa mlango ulofunguliwa; ninyi watu mlikuwa waaminifu kuhudhuria; wala Yesu hajashindwa ila alitutokea kila wakati, katika ishara ya wakati tunaoishi. Nami ninatumaini ya kwamba kufufuka Kwake, Utu Wake wa daima uliofufuka, Milele, na Uwepo Wake, umewashawishi kumpenda na kumtumikia kuliko mlivyopata kufanya maishani mwenu mwote, kukusudia moyoni mwenu kuishi waaminifu Kwake, na kuishi karibu zaidi, vizuri zaidi.

³² Nilisikia hadithi wakati mmoja niliyosimuliwa, kuhusu wakati walipokuwa na watumwa huku Kusini

³³ Walikuwa wakiwauza sokoni; na kadhalika, kama walivyofanya katika wakati wa watumwa. Wao, hao Makaburu, waliwaingiza, huku katika Kisiwa cha Jamaica. Ndipo watu hapa, waliwaingiza kwa magendo. Nao waliwanunua wawe watumwa, jambo ambalo lilikuwa ni halali siku hizo. Nao wangepitia kule na kuwanunua, nao wangejitafutia watumwa wazuri wazito, mbona, wangeninii. Wangemzalisha huyo mtumwa mkubwa mzito na mwanamke mzito; jambo ambalo lingelela mtu bora zaidi. Hiyo ndiyo sababu wao ni mabingwa wa dunia leo, katika mambo, katika kupigana kwao. Walikuwa tu wamezalishwa, kama ng'ombe, na kadhalika.

³⁴ Lakini basi tunaona mnunuzi, wakati mmoja, wakala alipitia kule apate kununua kwenye shamba moja ambako walikuwa na watumwa kama mia moja.

³⁵ Nao hao watumwa, walikuwa, walikuwa na huzuni. Ilibidi wawapige, kuwafanya wafanye kazi, kwa kuwa walikuwa mbali na nyumbani. Waliingizwa kimagendo, walikamatwa, wakapelekwa utumwani nao wakachukuliwa kimagendo. Nao iliwabidi kuwapiga, kuwafanya wafanye kazi, kwa kuwa walikuwa wamekufa moyo; wako mbali na makwao. Hawatamwona baba na mama tena. Kamwe hawatawaona wake zao na watoto wao. Lilikuwa ni jambo la kuhuzunisha.

³⁶ Basi wakala huyu, siku moja, alipitia huko shambani, akasema, “Je! una watumwa wangapi?”

Kasema, “Karibu mia moja.” Kasema, “Hebu waangalie.”

37 Ndipo akatoka akaenda kule waliko, naye akawaona, jinsi wote walivyokuwa . . . Lakini jamaa mmoja kijana, haikuwabidi kumpiga mijeledi. Kifua chake kilikuwa kimebenuliwa. Kidevu chake kiliinuliwa juu, barabara. Na kwa hiyo wakala huyo, yule mnunuzi, akamwambia huyo bwana wao, akasema, “Aisee, ningetaka kumnunua yule mtumwa.”

Akasema, “Loo, la. Hauzwi.”

38 Akasema, “Vema,” kasema, “je, yule mtumwa, hivi yeye ndiye bosi wa hao wengine?”

Akasema, “La, la, yeye siye bosi.”

Kasema, “Je! wewe unamlisha tofauti?.”

39 Akasema, “La. Wote wanalia kule jikoni, pamoja. Yeye ni mtumwa tu.”

Kasema, “Ni kitu gani kinachomfanya awe tofauti sana na hao wengine?”

40 Akasema, “Nilishangaa kwa muda mrefu, mimi mwenyewe, ni kitu gani kilichomfanya tofauti. Lakini siku moja nikagundua. Huko katika nchi ya uenyeji wake, mahali wanakotoka, Afrika, baba yake ni mfalme wa kabila lao. Na hata hivyo, akiwa yeye ni mgeni, anajua ya kwamba yeye ni mwana wa mfalme, naye anatenda kama mwana wa mfalme.”

41 Loo, jambo hilo linapaswa kutufanyia kitu gani! Ingawa tumetengwa mbali ugenini, ingawa tuko kwenye ulimwengu wenye giza wa kutokuamini, na huzuni na magonjwa na mauti, hata hivyo hebu na tutende kama wana na binti za Mungu. Sisi ni wana na binti wa Mfalme. Hilo linapaswa kubadilisha msimamo wetu, kila kitu. Haidhuru watu wengine wakoje, inatubidi kushikilia haki za Mungu. Tunakumbuka ya kwamba hapa sio nyumbani petu. Sisi si wa nchi hii. Sisi si wa ulimwengu huu. Tumezaliwa na Roho wa Mungu, ambaye yuko Juu.

42 Tulipokuwa tukienda, mke wangu hapa si muda mrefu uliopita, kwenye duka la chakula. Niliona jambo la ajabu katika msimu wa kiangazi, Indiana, mwanamke mmoja alikuwa amevaa gauni. Hawavai magauni tena, mwajua. Na kwa hiyo mke wangu akasema . . . Nikasema, “Vema, angalia pale. Sijui kama yule mwanamke ni Mkristo?”

43 Wakasema, “Vema, wanawake hawa wote; ninajua baadhi yao hapa, wanaimba katika kwaya makanisani.” Akasema, “Ni kwa nini, Bill, kwamba wanafanya jambo hilo?” Nikasema, ndiyo . . . “Na—na watu wetu hawafanyi jambo hilo.”

Nikasema, “Ndiyo. Sisi ni taifa tofauti.”

Akasema, “Sisi ni Wamarekani, sivyo?”

44 Nikasema, “Loo, la. Sisi tumefanya kambi tu hapa. Sisi si Wamarekani.” Nikasema, “Unaona, sisi tumetoka Juu.”

45 Roho Mtakatifu alishuka chini, akaiunganisha mioyo yetu na Mungu, nasi tukakiri, kama Ibrahimu, “Sisi ni wasafiri na wageni.” Hapa si nyumbani petu. “Tunautafuta mji ambao Mwenye kuujenga na kuubuni ni Mungu,” unaoshuka kutoka Juu. Naam, sisi ni wana na binti za Mfalme.

46 Sasa nitaleta jambo dogo ambalo linasikika la kuchekesha, kwa dakika chache tu, bali nitafanya kesi, kesi ya mahakamani hapa.

47 Je! mnaweza kunisika? Mnaweza kunisikia kutoka umbali gani, inueni mikono yenu. Vema, sawa. *Huku* nyuma, je! mnaweza kunisikia? Vema. Ninazungumza kwa sauti kuu, karibu, ninavyoweza.

48 Nitafanya kesi ya mahakamani, na kesi hiyo, ni, “Neno la Mungu, lililoahidiwa, dhidi ya ulimwengu.” Sasa tutafanya jambo hili kana kwamba ni kesi ya mahakamani, kwa kitambo kidigo, kabla ya ninyi kuja kwenye mstari wa maombi. “Neno la Mungu dhidi ya dunia,” sasa hiyo ndiyo kesi.

49 Sababu ya shitaka hili ni uvunjaji wa ahadi, ile ya, “Ahadi za Mungu,” wao wanadai ya kwamba, “Mungu hakutimiza ahadi Yake.”

50 Wakili mwendesha mashtaka katika kesi hii ni Shetani, naye ndiye shahidi wa dunia, kwa kuwa yeye ni wa dunia.

Mtetezi katika kesi hii ni Mwenyezi Mungu.

Shahidi mtetezi wa kesi hii ni Roho Mtakatifu.

Tutawaita kwenye kesi, kwa muda wa dakika chache tu.

51 Mashahidi wa mwendesha mashtaka, ambao anawaleta kutetea kesi yake, ni Bw. Kutokuamini, Bwana Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira.

52 Tutafanya kesi sasa. Mahakama inanyamazishwa sasa. Mwenye kuendesha mashtaka anamwita shahidi wake, Bw. Kutokuamini. Anasimama, kwanza.

53 Mngali mnaweza kunisikia? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sawa. Vema. Sasa ninaweza kujisikia nimetulia kidogo zaidi.

54 Sasa, mnaelewa, ni kesi dhidi ya Mungu, ya kwamba Bw. Kutokuamini na Bw. Mwenye Kushuku na Bw. Mkosa Subira wanampeleka Mungu ma—mahakamani, “kwa kuwa Yeye hatimizi Neno Lake,” wao wanasema. Vema.

55 Wakili mwendesha mashtaka katika kesi hii, yeye daima huiwakilisha nchi, na wakili mwendesha mashtaka katika hali hii ni Shetani mwenyewe. Naye ananinii . . .

Tunafanya kesi.

56 Vema, wanamwita wa kwanza kwenye kizimba cha shahidi kortini, huyo ni Bw. Kutokuamini. Analalamikia jambo hili, ya kwamba, “Neno lote lililoahidiwa na Mungu si la kweli.”

57 Sasa Yeye anashtakiwa kwa ajili ya jambo hili. Sikilizeni sasa kwa makini. Msilikose.

58 Anadai ya kwamba Marko 16, ambayo nimesoma sasa hivi tu, alihudumiwa hiyo kwenye mkutano ulioitwa wa Roho Mtakatifu ambako wengine walidai kuponywa. Na alihudumiwa kwa kifungu hicho, miaka miwili iliyopita, wala hakuna mabadiliko yoyote kwake bado, ya kwamba, “Ishara ‘hizi’ hazifuatani na mwaminio.” Yeye alisema alifanya dai hili dhidi Yake. Vema, anaketi chini.

59 Tunamwita shahidi anayefuata. Huyu ni Bw. Kushuku. Yeye anachukua Maandiko ya Neno la Mungu, ya Yakobo 5:14. Naye akasema ya kwamba alikuwa mahali fulani walipodai ya kwamba wazee waliitwa, naye akatiwa mafuta na kuombewa. Na hiyo ni zaidi ya mwezi mmoja uliopita, wala hapajakuwa na badiliko lolote kwake, kwa hiyo anajua ya kwamba hilo si sahihi. Anamwita Mungu, na kumshitaki Mungu, kwa ajili ya jambo hilo.

60 Shahidi anayefuata ni Bw. Mkosa Subira. Ni jamaa mbaya sana. Vema. Bw. Mkosa Subira, yeye anadai ya kwamba alisoma kutoka katika Neno la Mungu, katika Marko 11:22 na 23, ya kwamba wakati unapoomba, kama uliamini ya kwamba ulichoomba, unapokea, kitakuwa chako.” Naye anasema ya kwamba aliomba apate kuweka chini mikongojo yake, baada ya yeye kusoma Neno na kumwomba Mungu amponye. Na aliomba kuweka mikongojo yake chini, na hiyo imekuwa ni miaka mitano iliyopita, wala hajaweza kuiweka chini tangu wakati huo.

61 Kwa hiyo wao—kwa hiyo wao wanadai, “Mungu hana haki ya kuweka ahadi kama hizi zisizotimia katika Neno Lake.” Sasa je! mnaipata hiyo kesi sasa dhidi ya Mungu? “Yeye hana haki ya kufanya hivyo, kuweka Maandiko kama hayo ya Marko 11:23, 22 na 23, na Marko 16, Yakobo 5:14, na ahadi kama hizo.” Wanamshitaki Mungu kwa sababu ya kuvunja ahadi kama hizo, kwamba, “Yeye amevunja ahadi Yake, wala hawezi kuisimamia.” Nao wanamshitaki kwa kuweka hizo katika Neno Lake, kwa kuwa, “Watoto Wake waaminio hawatambulishwi pamoja na madai hayo, na hayo yanawafanya kuteswa, kwa kuwa hayatimii. Mungu hathibitishi Neno Lake baada ya Yeye kutoa ahadi.”

62 Loo, tuna kesi halisi hapa sasa. Ninawaangalia, jinsi wanavyoweza kushuhudia! Hata hivyo, sikilizeni mashahidi hao wakisimama tena na kusema, “Hata hivyo, sisi ni waamini!” Wanadai kuwa ni waamini, wenyewe eti. “Naye alisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’ ‘Kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule.’ ‘Ukiuambia mlima huu, “ng’oka” wala usitie shaka moyoni mwako, itatukia.’ Nasi ni waamini.” Na, hata hivyo, tena mtu anasimama na alisema, “Hata hivyo, Yeye, yaani Mungu, aliahidi kwamba mambo yote yanawezekana

kwa hao waaminio.” Ni shtaka la namna gani dhidi ya Mungu na Neno Lake!

⁶³ “Hata hivyo tena, Yeye anadai kuwa hai baada ya kusulibishwa. Na kudai ya kwamba Maandiko Yake katika Waebrania 13:8, ya kwamba Yeye ni Mungu tu namna ile ile leo kama alivyokuwa jana, na atakuwa hivyo milele.” Wazia tu juu ya Mungu yeye yule! Nao wanamshtakia jambo hilo, kwa sababu, “Sivyo ilivyo,” hawawezi kulifanya litende kazi ipasavyo. Vema.

⁶⁴ “Pia, ya kwamba anadai,” huyu ni mshtaki sasa, “yeye anadai ya kwamba mbingu na nchi zitashindwa, bali Neno Lake halitashindwa kamwe.” Hao wanapaswa kuwa ni waamini wanaozungumza. Sasa, ni shtaka la jinsi gani! Ni mashtaka ya jinsi gani tuliyo nayo dhidi ya Mungu, ya kwamba, “Yeye ametamka matamshi haya, wala si mkuu vya kutosha kusimama nyuma ya matamshi Hayo.” Unawazia nini juu ya jambo hilo?

⁶⁵ Na Shetani yule mshtaki ameketi pale, akiuwakilisha ulimwengu, kudai haya, uvunjaji wa ahadi kwa upande wa Mungu, kwa sababu, “Watu hawa wamekuja, wamehudhuria mikutano hii, na—na kukubali mambo haya ambayo Mungu aliyasema, kwamba yalikuwa ni ya kweli, na hata hivyo hakuna kitu chochote kimetendeka kwao.”

⁶⁶ Sasa, sasa hebu na tuwaache mashahidi wa mshtakiwa waketi chini kwa kitambo kidogo, unajua. Wana upande mwingine.

⁶⁷ Sasa tutamwita shahidi wa utetezi. Shahidi wa utetezi wa mshtakiwa, huyo ni Mungu. Shahidi wa utetezi wa Mungu ni Roho Mtakatifu. Mleteni asimame kizimbani. Hebu na tusikie ushuhuda Wake

⁶⁸ Jamani! Kwanza, anatahadharisha juu ya tafsiri potovu ya mshtaki ya Neno kwa watu. “Hiyo ni kweli, kwa kuwa yeye ndiye mfasiri yule yule ambaye Hawa alikuwa naye. Yeye ni mtafsiri yule yule aliyekuwa naye Hawa. ‘Loo, hakika, *Hili* ama . . . *Hili* ni sawa, bali *Hilo* si sawa.’ Unaona, mfasiri yule yule, ndivyo alivyo huyo mshtaki, maana yeye ni ibilisi. Yeye yule ambaye. . .”

⁶⁹ Mungu aliwakinga watoto Wake nyuma ya Neno Lake. Na mara ya kwanza kabisa unapotoka nyuma Yake, wewe ni shabaha ya ibilisi. Bali hawezi kukupata mradi tu umezingirwa na Neno.

⁷⁰ “Sasa ahadi ni kwamba . . .,” Yeye alisema mara nyingine tena, “Ninataka mwangalie.” Anasema . . . Sasa huyu ni shahidi wa utetezi, Roho Mtakatifu. Yeye alisema, “Ahadi hiyo ni kwa waaminio peke yao, si kwa wanaojifanya waamini na wenye kushuku na wasioamini. Ahadi ni kwa waaminio peke yao, si kwa hao wengine.” Sasa, huyu ni ninii—huyu ni shahidi wa utetezi. Na shahidi wa utetezi anapaswa kujua, kwa maana

Yeye ndiye anayelihiuisha kwao. Yeye anajua kama ni kweli ama si kweli.

⁷¹ Yeye pia anataka watu waone hapa, kwamba Yeye akiwa ndiye mwenye kulihuisha Neno, pia anataka watu wazingatie, kwamba, “Neno ni mbegu. Na kama mbegu ikiangukia kwenye ardhi nzuri, yenye rotuba, itazaa kile hasa Mungu alichosema itazaa. Bali isipoanguka kwenye ardhi nzuri, hivi kwamba hakuna udongo wa kutosha, imani ya kutosha, kuifanya mbegu hiyo iote.” Nafikiri, Yeye kwa kuwa Ndiye anayelihiuisha hiyo mbegu, Yeye anapaswa kujua. Je! hamdhani hivyo ndivyo ilivyo? Ni wangapi wanaoamini jambo hilo, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye Ndiye anayepaswa kujua. Yeye ndiye shahidi halisi hasa wa utetezi. Vema.

⁷² Mtetezi, akishuhudia sasa, ataita shahidi Wake wa kwanza. Sasa, unaona, mshtaki alimwita shahidi wake, Bwa. Kutokuamini, Bwana Kushuku, na Bw. Mkosa Subira. Sasa shahidi wa utetezi ana haki ya kuita mmoja wa mashahidi Wake. Roho Mtakatifu ana haki ya kumwita, maana Yeye ni shahidi wa utetezi wa Neno la Mungu.

⁷³ Sasa, watu hawa wanadai ya kwamba wanaamini, bali Roho Mtakatifu hajui kitu juu ya jambo hilo, na Yeye ndiye pekee anayeweza kulihuisha. Ni kama tu vile mwili wako hapa ulivyo, unaona, mwili wako umekufa bila roho, vivyo hivyo na Neno la Mungu limekufa bila ya Roho Mtakatifu kulihuisha. Roho huhuisha mwili, na Roho Mtakatifu hulihuisha Neno. Mnalipata? Sasa, Yeye anapaswa kujua.

⁷⁴ Sasa Yeye atamwita shahidi wa kwanza. Hebu na tuone ni nani atakayemwita. Nuhu, Yeye atamwita Nuhu.

⁷⁵ Nuhu alisema, “Siku nilizoishi zilikuwa ni wakati wa sayansi,” walikuwa werevu kwa mbali sana kuliko walivyo leo. “Na Bwana Mungu aliniambia mvua itanyesha kutoka mbinguni.”

⁷⁶ Kulikuwa hakujawahi kunyesha kamwe, mnakumbuka, juu ya nchi. Nao wangeweza kuchukua zana za sayansi na kuthibitisha hakukuwa na mvua huko juu. Kumbukeni, haikunyesha kamwe katika siku hizo. Mungu aliitia ardhi maji kwa kumwagilia.

⁷⁷ Lakini yeye alisema, “Kutanyesha mvua na dunia itagharikishwa. Kutakuja gharika kuu, kote duniani, ambayo itaifunika na kuigharikisha” Yeye alisema, “Hata hivyo, nilipewa maagizo kutoka kwa Mungu, kujenga safina. Niliingia kazini kuijenga safina hii, nikionyesha imani yangu, ya kwamba niliamini yale Mungu aliyosema kwamba yalikuwa ni Kweli, haidhuru sayansi ilisema nini kuhusu jambo hilo.” Nafikiri yeye ni shahidi mzuri, mwaonaje? [Kusanyiko linasema, “Amina”—Mh.] Na haidhuru mtu mwingine yeyote anasemaje juu ya jambo hilo, Mungu alisema ya kwamba kutanyesha; kwa hiyo kama

hakujapata kuwa na mvua kule juu, Yeye anaweza kuweka mvua kule juu. Nitaijenga safina, hata hivyo, nikijiweka tayari kwa ajili yake.

⁷⁸ “Ingawa, nilikuwa na jamaa huyo, kwenye kizimba cha ushahidi hapa muda mfupi uliopita, Bw. Kutokuamini, alinidhihaki daima. Alinifanyia dhahaka. Nami nilimwona Bw. Kushuku; alikuja na kunicheka. Bw. Mkosa Subira, wote hao, walinicheka, kwa kuamini mwujiza kama huo. Lakini, mimi nilingojea. Wakati nilipomaliza hiyo safina, mvua kamwe haikuja. Nami nilingojea kwa muda wa miaka mia moja na ishirini, kabla haijakuja, bali ilikuja.” Amina.

⁷⁹ “Keti chini, shahidi. Huo ni ushuhuda mzuri. Hebu na tumwite mwingine, shahidi namba mbili. Ibrahimu, mleteni huku.” Sasa hivi tu tulikuwa tukizungumza juu yake.

⁸⁰ “Pia,” yeye akasema, “mimi nilisikia Neno la Mungu, nilipokuwa na umri wa miaka ishirini na mitano, likiniambia jambo lililokuwa kabisa haliwaziki. Lilibidi liwe ni mwujiza mkubwa mno mara mkubwa mno. Ya kwamba, nitazaa mtoto mwanamume na mke wangu, mwenye umri wa miaka sitini na mitano, wakati yeye alipokuwa na umri wa miaka sitini na mitano. Tulianza kuweka kila kitu tayari, kwa maana Mungu alisema hivyo. Tuliamini jambo hilo. Na ninii. . . Niliwaambia marafiki zangu wote ya kwamba mambo haya yatatukia, baadaye. Ilibidi haya yatukie kwa sababu Mungu alisema hivyo. Nilingojea kwa subira. Mwezi wa kwanza ulipokuja, nilimwuliza mke wangu jinsi alivyokuwa akijisikia. ‘Hakuna tofauti.’ Vema, nilimwamini Mungu hata hivyo.

⁸¹ “Kulikuwa na Bw. Kutokuamini, Bw. Dhahaka, Bw. Kushuku, na wote hao wakiwa wamesimama karibu. Walinidhihaki na kunicheka, wakaniita, ‘Baba wa mataifa,’ wakati sikuwa na watoto.

⁸² “Nami ninaendelea kuamini kila mwezi, kila mwezi lingetukia. Alizidi na kuzidi kuzeeka wakati wote, bali ilinini. . . katika miaka ishirini na mitano baadaye, Mungu alitimiza Neno Lake. Ilitendeka.”

⁸³ “Ibrahimu, huo ni ushuhuda mzuri. Neno halikusema ni *lini*; Yeye alisema ya kwamba angempa. Alisema, ‘Nitakupa mtoto, wa kiume, kwa Sara.’ Si mwezi ujao; hakusema kamwe mwezi ujao. Alisema angempata; hakusema *lini*. Wao, maombi. ‘Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.’ Wazo ndilo hilo. ‘Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, na Mungu atamwinua.’ ‘Kaeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mtakapovikwa Uweza, utokao Juu.’ Si kwa siku moja, saa mbili, siku kumi, miaka kumi. ‘Mpaka Nguvu zitakapokuja!’” Shahidi halisi wa utetezi, ndivyo walivyo mashahidi hawa! “Yeye hakusema kamwe ni *lini* tutakapopata mtoto huyo,” Ibrahimu alisema, “bali Yeye alisema tutampata. Na wakati huo

wote mambo yalikuwa yanazidi kuwa magumu dhidi yangu, nilikaa tayari. Kwa maana, sikusitasita katika kutokuamini kwa hao watu. Nilishikilia moja kwa moja.”

⁸⁴ “Vema, Ibrahimu, keti chini. Sasa hebu na tumchukue shahidi mwingine, shahidi namba tatu. Hebu tumlete Musa, tuone vile anavyosema.”

⁸⁵ “Sasa,” yeye alisema, “mimi nilikuwa mwanasayansi. Nilikuwa nimekaa miaka arobaini nyikani, baada ya kushindwa na kazi. Lakini siku moja nilikutana na Mungu. Na Sauti hiyo, Nguzo ya Moto huko mbali nyikani, iliniambia, Sauti ya Kimaandiko, ya kwamba wakati ulikuwa umewadia, ya kwamba Yeye alikuwa amesikia kilio cha watu Wake, alikumbuka ahadi yake, Naye alikuwa akishuka kwenda kuwakomboo, Naye alikuwa akinituma kwa ajili ya kazi hiyo.

⁸⁶ “Nilimwomba anipe ishara. Alinipa ishara, kisha akanipa ishara nyingine; ishara zote mbili zingekuwa na sauti. Alisema, ‘Basi wasipoamini ishara hizo zote, mwaga tu maji (kutoka baharini) juu ya nchi, nayo yatakuwa damu.’ Naam, hakuna lingine. Farao alikuwa amekwisha mambo yake, kasema, ‘kama, wewe, wao hawataamini ishara hizo, sauti hizo.’

⁸⁷ “Na, hata hivyo, nilishuka nikaenda kwenye wajibu wa huduma, kama tu vile Mungu alivyoniambia kufanya. Yehova, yule MIMI NIKO, alivyoniambia nishuke niende na kufanya ishara hii. Ndipo nilichukua nikapeleka ishara hii mbele ya mchungaji Farao, na nikatupa fimbo yangu chini. Na unajua nini? Alijaribu kulifanya lionekane ni jambo la udanganyifu, kama vile kwamba ilikuwa ni vitimbi vya kiuchawi. Naye akawachukua waigaji wa kimwili watoke waende walidhihaki hilo, wakafanye jambo lile lile. Bali nilijua lilikuwa ni Neno la Mungu, nami nilikuwa nimekuja kuwatoa hao wana kule. Haidhuru ni jambo gani lililotukia, ningali niliendelea kuamini Neno la Mungu, kwa hiyo nililishikilia imara.” Sina mengine!

⁸⁸ Musa, wewe ni shahidi halisi! Haileti tofauti yoyote, wanajaribu kuliiga, na kujaribu kufanya jambo fulani, kulifanya lionekane kana kwamba ndilo lenyewe, alishikilia imara. Wachawi walijitokeza. “Unaona,” Farao akasema, “unaona, ni vitimbi fulani rahisi. Ni Beelzebuli, telepathia fulani ya kiakili ama kitu fulani. Nina watu hapa, wachawi, wanaoweza kufanya jambo lile lile, waaguzi, kulidhihaki, chochote kile.” Hilo halikumkomesha Musa. Lilikuwa ni Neno la Bwana, kwa maana ilifuatwa na ishara ya Kimaandiko.

⁸⁹ “Loo, naam,” kasema, “Bw. Kutokuamini, Bw. Kushuku, na hao wote, walining’inia mabegani mwangu. Bali nilidumu moja kwa moja na Neno hilo, nikijua ya kwamba Mungu ndiye aliyesema hilo Neno. Mungu alihusika kulishughulikia; si wao. Aliniambia nilipaswa kuwachukua hao wana niwapeleke kwenye nchi ya ahadi. Aliniambia nitawatoa, nilikuwa niwatoe

huko, na nilikuwa nirudi kwenye mlima huu ambapo jambo hilo lilitukia. Sijui ni jinsi gani. Farao alitisha—aliyatishia maisha yangu, na kila kitu kilitukia, bali nilidumu mwaminifu kwa ile ahadi. Hatimaye, Mungu alimshinda huyo adui, nami nikawatoa kupitia katika Bahari ya Shamu, kama kupitia katika nchi kavu. Mungu alidumisha ahadi Yake, nami nilikuja moja kwa moja mpaka kwenye mlima ambapo aliniambia ningekuja, mlima ule ule.” Unaona, Yeye alikuwa ameamini ya kwamba ilikuwa ni Mungu, naye akashikilia imara.

⁹⁰ Hebu na tumlete shahidi namba nne, kwa kuwa tuna haraka. Hebu na tumlete shahidi namba nne. Yoshua, ambaye alipachukua mahali pa Musa.

⁹¹ Yoshua alisema, “Nilishuka nikaenda kule na wapelelezi. Nilitumwa. Tulitumwa tukiwa watu kumi na wawili; mmoja kutoka katika kila madhehebu.” Akaongeza kusema, “Tulishika njia tukaenda kule na tukaangalia. Na hawa hapa wanarudi, wameogopa, na kusema, ‘Vema, tunaonekana kama panzi, tukilinganishwa na jamaa hao. Loo, jamani, wao ni wakubwa zaidi kuliko sisi! Na watu wenye nguvu, jinsi hao wote walivyo! Tunaonekana kama panzi.’” Kisha akasema, “Huko Kadeshi-barnea niliwatuliza watu, kasema, ‘Hebu kidogo. Mnawaangalia hao majitu na upinzani. Mimi ninaangalia ahadi ya Mungu. Mungu alisema, “Nitawapa hiyo nchi.” Amina. Nikawanyamazisha watu, kwa maana Neno liliahidi jambo hilo.”

⁹² “Ndipo, siku baada ya siku, walisogea karibu na kusema, ‘iko wapi hiyo nchi? Yako wapi maziwa na asali, Yoshua? Uliahidi jambo hilo, pia. Liko wapi?’ ‘Mungu atalishughulikia.’ Naye akaacha hao wasioamini wote wafe. Alinibakiza hai, akakiinua kizazi kingine. Miaka arobaini baadaye, tukaiteka hiyo nchi. Mungu alisema hivyo!”

⁹³ Na, kumbukeni, walikuwa umbali wa safari ya siku mbili tu. Yeye aliwazuia kwa muda wa miaka arobaini kwa sababu ya kutokuamini kwao. Uponyaji wako huenda usiwe umbali wa dakika tano. Kutokuamini kwako kutakuzuia usikupate mradi ungali hai. Huna budi kuamini hilo! Yeye ni shahidi halisi, Yoshua. Naam, bwana. Waliiteka hiyo nchi, miaka arobaini baadaye.

⁹⁴ Tuna mashahidi wengi sana ambao tungaliweza kuwaita, lakini, kama mtaniruhusu, mimi ningetaka kuwa shahidi Wake anayefuata. Ningetaka kujitolea kuwa shahidi Wake, endapo hilo halitasikika la kibinafsi sana. Mimi ni shahidi Wake. Ninataka kuwa nanii Wake anayefuata, shahidi Wake wa tano.

⁹⁵ Mungu anawezaje kuchukua gugu na kufanya punje ya ngano kutoka kwake? Mwenye dhambi, aliyetoka katika familia yenye dhambi; wote wakiwa na bunduki, na wakafa wamevaa

buti zao; watengenezaji gongo na chochote kile. Mbona, mimi sikuwa na uhusiano wowote na jambo hilo.

⁹⁶ Mama yangu aliye Utukufuni leo, alisema, ile saa niliyozaliwa, Malaika wa Bwana alikuja dirishani na akasimama juu ya kitanda kidogo cha mtoto nilipokuwa. Wana picha yake katika kumbi za kisayansi za Sanaa za masomo ya Dini leo. Inajulikana duniani kote. Mungu aliahidi kufanya mambo haya. Nilipokuwa mvulana mdogo, sauti ilisema na mimi, ikasema, “Usivute sigara kamwe, kutafuna, wala kunywa pombe, kuuchafua mwili wako kwa njia yoyote. Kutakuwako na kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima.” Lilinitisha, kwa kweli.

⁹⁷ Nilijua kitu gani juu ya dini? Ukoo wangu, hapo zamani, walikuwa ni Wakatoliki. Nilijua je jambo lolote kuhusu mambo haya? Sikuwahi kuwa na kanisa maishani mwangu. Wote wawili walifunga ndoa nje ya kanisa, kwa hiyo walininii tu... Mama na baba, wote wawili, walikuwa ni Waairishi, na kwa hiyo walifunga ndoa tu nje ya kanisa, nasi hatukuwa na dini.

⁹⁸ Tuliishi tu kama kundi la mbwa, tulikuwa na mkokoteni mdogo, kama wa wasafiri wa likizo wapiga kambi, watangitangi, popote ambapo tuliweza kupata kibanda kidogo tungeweza kukodi kwa dola tatu ama nne kwa mwezi. Hivyo ndivyo tulivyoishi.

⁹⁹ Maskini mvulana mdogo asiye na viatu, akibeba maji kupeleka kwenye kikeneko cha wiski, siku moja; wakati Mungu, katika ukuu Wake, akali akidumisha Neno Lake, alishuka katika upepo wa kisulisuli na kusimama pale, na kusema, “Usifanye mambo haya.” Alisema jambo hilo. Nilipokuwa kijana mvulana, maono yalianza kutokea machoni mwangu, tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Yaliniogofya. Nikaokoka, ndipo nikajiunga na kanisa la Kibaptisti. Nikaauliza...

¹⁰⁰ Niliwaambia ndugu zangu Wabaptisti juu ya kwenda... Sikujua jinsi ya kuita kitu hicho, ono. Nilikiita njozi. Ndipo nikaenda nikawaambia ndugu zangu kuhusu jambo hilo. Wao wakasema, “Billy, usijihusishe chochote na jambo hilo. Huyu ni ibilisi. Huyu ni ibilisi. Usijihusishe kitu na jambo hilo.”

¹⁰¹ Usiku mmoja, kwenye kambi ndogo ambako nilikuwa nikivua samaki, huko mbali kabisa milimani, nilikuwa nimelala huko mbali msituni. Yapata saa tisa usiku mmoja, niliona Nuru ikija. Nilikuwa tu mimeacha kusoma Biblia. Nilifikiri ilikuwa ni mtu fulani alikuwa anakuja akimulika kupitia shimo la kifundo, kwa taa ya fanusi au kitu fulani. Ilikuwa ni huko mbali msituni. Nami nilidhani ni mtu fulani alikuwa anakuja. Nuru hiyo ilikuwa inaangaza hapo sakafuni; ikapanuka na kuzidi kuwa kubwa. Nikasikia Mtu akitembea. Alipotokea, ilikuwa ni Mwanadamu. Hakuwa na viatu. Alikuwa na nywele zilizofika

mabegani Mwake, na alikuwa amevaa joho. Na iliniogopesha nusura kufa.

¹⁰² Akasema, “Usiogope. Nimetumwa toka Uweponi mwa Bwana Mungu, kukwambia hayo, maisha yako ya kipekee. Usijaribu kuyakwepa mambo haya. Huo ni wito wako. Na Mungu atakuwa akikutuma mahali mbalimbali kote duniani, kuwaombea wagonjwa. Na kama utawafanya watu kuamini na kuwa waaminifu, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi.”

¹⁰³ Liliniogopesha nusura kufa. Kwa kweli, liliniogopesha. Nilisimama pale, naye—naye akaendelea kuzungumza. Nikasema, “Bwana, niko hapa kwa ajili ya njozi hizo na vitu kama hivyo.”

¹⁰⁴ Akasema, “Kutakuwa na mambo matatu yatakayotukia. Kwanza, utajua kwa kuchukua mkono wako kuwashika watu. Ndipo itakuwa, baada ya hayo, kama ukiwa mwaminifu, kwamba utajua siri za moyo wao.”

¹⁰⁵ Ndipo nikasema, “Hilo ndilo limenileta hapa kuzungumzia, ilikuwa kwamba mimi . . . Ndugu zangu waliniambia ya kwamba jambo hilo lilikuwa ni la ibilisi. Mimi ni Mkristo. Sitaki kuwa wa ibilisi hata kidogo.”

¹⁰⁶ Akasema, “Kama ilivyokuwa huko zamani, ndivyo ilivyo sasa. Wakati walipokuwa wakibishana kwamba ni vifungo vya aina gani wanavyopaswa kuvaa kwenye makoti yao, na mambo kama hayo, na wahudumu wakisema ya kwamba Paulo na hao wengine wanaupindua ulimwengu, ilikuwa ni kitu gani? Lakini ilikuwa ni pe—pepo mchafu aliyesema, ‘Watu hawa ni watumishi wa Mungu, ambao wanaupindua ulimwengu.’ Hiyo Paulo na hao wengine waliyohubiri. Na pepo mchafu akashuhudia ya kwamba wao walikuwa watumishi wa kweli wa Mungu.”

¹⁰⁷ Aliniambia, akasema, “Hivi hukumbuki, katika Maandiko, hilo ndilo jambo ambalo Bwana wetu alifanya? Na hilo ndilo aliloahidi, alisema lingetukia tena katika siku za mwisho.”

Nikawaza, “Vema, hilo linaweza kuwa ni kitu gani?”

¹⁰⁸ Akasema, “Vema, ni Roho wa Bwana Yesu. Yeye ni Neno. Naye ameahidi jambo hilo katika siku za mwisho. Sasa usiogope.”

¹⁰⁹ Basi nilishuka nikaenda kulibatiza kundi la watu mtoni. Nilipokuwa nikibatiza kule, ambako kama watu elfu tano walisimama ufukoni; katikati ya mchana, saa nane alasiri; ni joto, hawakuwa wamepata mvua kwa juma moja ama mbili; nami nimesimama ukingoni. Hii hapa ile Nguzo ya Moto inakuja ikizungukazunguka kutoka hewani, ikishuka kuja mahali nilipokuwa nimesimama, na Sauti ile ikisema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa, na kutangulia kuja kwa

kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia Kuja kwa Pili kwa Kristo.”

¹¹⁰ Magazeti yaliandika habari hiyo, na jambo hilo likasambaa mpaka huko Canada kwenye Shirika la Magazeti, kote ulimwenguni, “Mhudumu mmoja wa mtaani, mhudumu Mbaptisti, akiwa anabatiza, na,” yakasema, “Nuru ya ajabu inatokea juu yake.” Ile ile waliyopiga picha Yake hapa, na wakaichukua huko Ujerumani na—na kila mahali. Na imefanyika hivyo.

¹¹¹ Mchungaji wangu aliniambia, akasema, “Billy, ulikuwa na ndoto ya aina gani? Mbona, unajua wewe hukuona . . .”

Nikasema, “Kulikuwa na mamia waliokuwa wamesimama pale, walioshuhudia jambo Hilo.”

¹¹² Nao wangekuja kwangu, wakasema, “Loo, huo ni udanganyifu wa akili.” Akijaribu vizuri awezavyo, huyo ni maskini mzee Kutokuamini na Bw. Kushuku.

¹¹³ Nilishikilia moja kwa moja kwenye Neno. Nilidumu pale, kwa kuwa nilijua ilikuwa ni ahadi ya Mungu. Amina. Luka mlango wa 17, Yeye aliahidi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Nilipoona ulimwengu ukizidi kuchafuka, jinsi ulivyokuwa ukichafuka, nilijua jambo fulani halina budi kutimia. Niliona katika Malaki 4, ambapo wangeirudisha “Imani kwenye Neno,” ambayo walitoka kwake wakatawanyika. Nilijua jambo hilo lilikuwa halina budi kutimia, nami nilidumu mwaminifu kwa Neno. Ninamwona Yesu Kristo, leo, “ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Kusanyiko, inanyesha. Nitakoma papa hapa.

¹¹⁴ Ninataka kusema jambo hili. Nimewaleta mashahidi hawa wote; ushahidi wangu mwenyewe. Wengi wenu ni mashahidi, juma hili. Kitu hicho ni kweli, huu Ujumbe. Ninawezaje . . .

¹¹⁵ Daktari Davis aliniambia, “Eti mvulana, elimu ya msingi, akienda kuwaombea wafalme na watawala, na kuanzisha ufufuo utakaoenda kote duniani? Billy, jirudie.”

¹¹⁶ Lakini, ilitendeka! Ilitendeka! Miaka thelathini na tatu baadaye, ufufuo umekwisha, na ilitendeka. Mungu alisema hivyo! Mimi ni shahidi Wake. Yeye hakusema ni *lini* angefanya jambo hilo. Alisema angefanya hivyo! Nilingojea wakati ambapo Neno lingekuwa dhahiri sana, liwekwe mkononi mwangu, kama, Upanga, na hapo ningetambua kwa hilo mawazo hasa yaliyo katika moyo wa watu. Nikawazia, “Hilo linawezekanaje?” Nilingojea, nikiamini jambo hilo, nalo lilitukia. Mfanya Dhihaka, Asiyeamini, Mwenye Kushuku, Mkosa Subira, wangali wanangojea na kuangalia. Lakini Mungu, baada ya miaka thelathini na mitatu, amethibitisha jambo hilo, kwa wote, kote ulimwenguni. Ambapo magazeti ya kila siku, magazeti, na makala, yameandikwa, kote ulimwenguni.

¹¹⁷ Amua mwenyewe. Mawazo yako ndiyo baraza la wazee wa mahakama. Kila mzee wa baraza hana budi kujiamulia. Ninafunga mahakama. Toa hukumu wewe mwenyewe. Mawazo yako ndiyo baraza la wazee wa mahakama. Na matendo yako tangu sasa na kuendelea, alasiri ya leo, tutakapoweka mikono yetu juu ya wagonjwa, jambo hilo litadhihirisha jinsi uamuzi wako ulivyokuwa. Jinsi unavyotenda baada ya kuombewa, hilo litaonyesha jinsi nia yako ya kiakili ilivyoamua, yale wazee wa baraza la mahakama ya akili zako wameamua. Hilo litaonyesha kabisa, matendo yako tangu sasa.

¹¹⁸ Ninatangaza ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninatangaza hakuna kitu kinachoweza kusimama Mbele Zake; wanaume na wanawake watakaoamini. Je! Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹¹⁹ Bwana, Yesu, twaomba neno moja tu kutoka Kwako sasa, kuwafanya watu waamini. Wameketi hapa. Sikuwa nikitaka kwenda kufanya jambo hili, Baba. Bali, wamekuwa na subira sana, ninaomba sasa. Hivi hutaliruhusu, kwa ushahidi wangu mwenyewe?

¹²⁰ Tunaweza kusoma katika Biblia, ushahidi wa hao watu, ushahidi wa wasioamini. Tunaona mahali ambapo wao daima wamelihukumu. Hao Mafarisayo, watu wa dini katika siku hizo, walimhukumu Yesu Kristo. Lakini ilitibitika, Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Wao walisema, “Unajifanya Mwenyewe Mungu.” Yeye alikuwa Mungu. Alitenda kama Mungu; alihubiri kama Mungu; Aliponya kama Mungu; alifuka kutoka kwa wafu kama Mungu; alipaa Juu kama Mungu. Yeye ni Mungu. Yeye anakuja, Mungu. Tunaamini hilo. Katikati ya shida zote, Wewe ungali Mungu. Ushahidi Wako unaonekana wazi, Bwana.

¹²¹ Ninatoa ushahidi wa, ama nilinena kuhusu ushahidi wa watu hawa wengine. Maelfu mara maelfu ningeweza kuwaita, kwa pande zote mbili; mwenye kushuku, asiyeamini, na mtu yule ambaye hawezi kamwe kungojea muda mrefu vya kutosha. Wewe kamwe hukusema ni *lini*. Ulisema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, kama wakiamini, watapona, haidhuru ni wakati gani. Hukumwambia Ibrahimu ni wakati gani mtoto angezaliwa. Hukumwambia Musa kamwe ni siku gani angewarudisha watu hao kwenye mlima huo. Hukumwambia Nuhu ni siku gani mvua ingenyesha. Hukuwaambia kamwe ni wakati gani maalumu; wala Wewe hukutwambia.

¹²² Wewe ulisema, “Kama unaweza kuamini! Kama ukiuambia mlima huu, usitilie shaka moyoni mwako, yatatimia, yale uliyosema. Kama ukiamini jambo hilo!” Wewe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Bwana, nimelirudisha moja kwa moja kwenye mapaja ya watu. Ni juu yao.

¹²³ Nimewathibitishia, kwa Biblia, nasi sote tunajua jambo hilo, ya kwamba Upatanisho umefanywa. “*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu. Kwa mapigo Yake *sisi tuliponywa*.” Ni wakati uliopita, kufunga mdomo wa mwenye kushuku, na asiyeamini ambaye alisema Yeye hakufufuka, na kujaribu kulifanya hilo ni namna fulani ya Mungu wa kihistoria katika dini.

¹²⁴ Bwana, ninaomba ya kwamba utajitokeza, Yeye tena alasiri ya leo miongoni mwetu, na kulithibitishia kusanyiko hili ya kwamba Wewe upo hapa; Yeye aliyenena Neno, Mungu ambaye tumekuwa Naye mahakamani. Kwangu mimi, Wewe umehesabiwa haki, Bwana Mungu. Umejithibitisha Mwenyewe, Mungu. Jidhihirishe sana, kusudi kila mwanamume na mwanamke, maskini watu hawa wanaoketi hapa katika kibanda hiki kinachovuja sana, wakijaribu kulisikia Neno, lifanye halisi sana kwao, Baba. Jionyeshe Mwenyewe kuwa ni Mungu miongoni mwetu!

¹²⁵ Jinsi ambavyo watu katika nyakati zote, limekuwa kwa namna fulani ni geni, kwa watu. Wakati walipokuwa baharini usiku huo, Na—Nawe ukawajia, walifikiri alikuwa ni roho. Walikuwa... Hawakujua ilikuwa ni kitu gani, nao wakapiga makelele. Lakini ile Sauti ikarudi, “Ni Mimi.”

¹²⁶ Sauti ya Maandiko inanena, alasiri ya leo, ya kwamba muda ndio huu, wakati ndio huu, Sodoma na Gomora na mambo haya mengine yote yamekaa jinsi hasa yalivyopaswa kukaa. Wewe upo hapa, ukiuonyesha Uzao wa kifalme wa Ibrahimu ya kwamba Wewe u hai, na Mwana wa Adamu anafunuliwa katika siku hii ya Sodoma. Baba wa Mbinguni, jalia ya kwamba hawa watu wataona; na, watakapopita, ya kwamba watalichukua Neno la Mungu kama tu Ibrahimu alivyofanya. Haidhuru ni lini huyo mtoto mchanga...

¹²⁷ Tungeweza kumwita Isaya jukwaani, na Isaya angeweza kushuhudia. Angeweza kusema, “Bwana aliniambia, ‘Bikira atachukua mimba.’” Kama angaliweza kufufuka na kuzungumza na sisi alasiri ya leo, hapana shaka ila angesema, “Kila msichana mdogo wa Kiebrania, kwenye siku zangu zote, alitazamia kupata mtoto kwa Roho Mtakatifu; kila mmoja. Bali ulisema jambo hilo, ukaagiza liandikwe. Ulimitambulisha kama nabii Wako. Na maneno yangu niliyosema yaliungwa mkono na Wewe. Maono yangu yalikuwa ni ya kweli. Na hao watu waliyaamini, kwa kizazi kimoja ama viwili, kisha yakasahaulika. Hata hivyo, baada ya miaka mia nane, bikira alichukua mimba na mtoto akazaliwa. Jina Lake lilikuwa ‘Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, na Baba wa Milele,’ miaka mia nane baadaye.”

¹²⁸ Ee Bwana Mungu, ni nini kimewapata watu hawa, watu wetu juu ya dunia hii siku hizi, kujiita wenyewe Uzao wa kifalme wa Ibrahimu? Wakati, yeye alingojea miaka ishini na mitano,

akitumaini na—na akiwa na imani dhidi ya yasiyowezezana, kuona mwujiza ukitendeka, Nawe uliufanya. Ni zaidi sana vipi tunavyoweza kulichukua Neno Lako, wakati Wewe ukiwa ndiwe Mungu yeye yule anayeonekana ambaye alimtokea Ibrahimu, ambaye anajitokeza hapa kwetu katika mwili wa kibinadamu, kwa njia ile ile uliyomtokea Ibrahimu! Mungu, jalia ya kwamba wao watafanya hivyo, kila mtu, ataona jambo hilo alasiri ya leo, na wafanikiwe. Kila wakati watu wanapopita, na kuwekewa mikono, jalia waondoke kwenye jengo hili, wakifurahia, wala wasilighairi, bali waamini kama Ibrahimu na hao wazee wengine wote. Ulisema jambo hilo lingetukia, nalo litatukia kama hawatakufa moyo. Tujalie hilo, katika Jina la Yesu. Amina.

¹²⁹ Ninaamini. Ninaamini. Ninyi aminini! Ninaami ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Ninaamini ya kwamba amefufuka katika wafu. Ninaamini Yeye anaweza hata na zaidi kutimiza ahadi yoyote aliyoahidi kufanya. Yeye anaweza kutimiza kila neno alilopata kusema, Naye atalifanya kwetu hapa alasiri ya leo kama tu tutaliamini.

¹³⁰ Sasa, Yeye kamwe hakusema, “Basi enendeni, na—na mshtue watu kwa mkutuo kwenye viti vya magurudumu, na kuwachukua wagonjwa wa moyo na kufanya jambo *hili*.” Hakusema jambo hilo.

¹³¹ Kasema, “Wekeni mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Hao ni waamini.

¹³² Sasa, Roho Mtakatifu ndiye shahidi Wake wa utetezi hapa, Yeye anajua kama unaamini au huamini. Usije tu, ukibahatisha. Chukua huko kubahatisha, na uchukue tumaini hilo, na uchukue mawazo hayo, na uyaweke chini ya miguu yako, na kusema, “Nina imani, ninajua itatendeka!” Jambo fulani litatukia.

¹³³ Unafikiri ni kitu gani, kwangu mimi, kusimama hapa, enyi marafiki? Mnafikiri nini, kwangu mimi, kusimama hapa kama ilivyo sasa, mbele ya makusanyiko mara nyingine yanayofikia maelfu, na mamia ya maelfu, ningetoa dai ya kwamba Yeye yu hai, na Roho Wake aliniambia hivyo, Neno ambalo angenipa? Je! Mungu angeweza kufanya jambo lolote bila kuweza kulitimiza? Unaona, aliniambia atafanya jambo hilo! Hilo ni Neno. Na kusimama hapa mbele ya wasikilizaji, ambapo wenye kushuku, wasioamini, na wowote wale wameketi, kwa makumi elfu; na hata hivyo kumwona Yeye, kumwita jukwaani.

¹³⁴ Je! mnaamini Yeye yupo hapa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

¹³⁵ Mtu fulani aliye karibu. Si marafiki zangu sasa; kama wewe—kama wewe ni mgonjwa, mtu yeyote, marafiki zangu. Ni wangapi, papa hapa mbele yangu, wanaojua ya kwamba siwajui, inueni mikono yenu namna *hii*. . . ? . . .

¹³⁶ Sasa wapo wengine hapa wanaonijua mimi. Unaona, mahali fulani *hapa*, wananijua mimi, papa hapa. Hiyo ni kweli, sivyo,

ndugu, ninyi nyote sehemu hiyo hapo? Unaona? Angalieni huku. Unaona, wananjua.

Lakini *humu* ndani, hamnijui mimi.

¹³⁷ Ni wangapi kwenye safu hii moja hapa hawanijui, inueni ninii yenu. . . Je! yupo mtu yeyote kwenye safu hizi tatu hapa, papa *hapa* ndani, ambaye ananjui mimi; anayejua ya kwamba ninajua jambo fulani kukuhusu wewe, na kila kitu? Inueni mikono yenu.

¹³⁸ Je! huko nyuma *ninyi* ninawajua? Ninakujua *wewe*, ndugu? Siamini yeye alinieleva, maana mimi simjui. Yeye hanihui mimi. La. Hunijui mimi, siyvo, bwana? U—u—unanijua? Hivi unajua ya kwamba ninajua shida yako? Naam, wewe ni nani? Labda. . . Hanielewi, maana si—simjui mtu huyo. Sasa uli- . . . Je! unajua ya kwamba ninajua shida yako; bila ya kuwa wa kiroho, ninakujua tu kama mwanamume, na ninajua una shida gani? [Ndugu huyo anasema, “La.”—Mh.] La hasha. Hakika. Unaona, nisingefanya hivyo. Unaona, inanyesha, nawe huwezi kuelewa.

¹³⁹ Roho Mtakatifu na atusaidie sasa. Vema, tukianzia sehemu *hii* basi. Je! mnaamini, upande *huu*.

¹⁴⁰ Mtu huyo mmoja, sasa, yeye huenda hata ni—nisijue. Mtu yule anayeketi pale, ameinua mkono wake, unaona, sidhani. . . Yeye hanihui. Ninajua hanihui. Lakini ameweka tu. . . alikuwa ameinua mkono wake juu, hata hivyo. Sitamgusa, basi, unaona. Mimi. . .

¹⁴¹ *Kweni* nyote. Bwana awabariki. Mtu fulani na aombe, *hapa* ndani. Je! mnaamini? Kila mmoja wenu, je! unamwamini? Kwa moyo wako wote, amini.

¹⁴² Huyu hapa maskini mama mmoja. Hebu nimwite tu mtu mmoja, nianze kuzungumza, nizungumze tu na mtu fulani; kupata ninii Yake. . . tumwache Roho Mtakatifu afanye kazi. Maskini yule mama anayeketi pale, je! unaniamini kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu? Wewe, maskini mama unayeketi papa hapa. Unaona? Wewe, vema, ninyi wawili mlitikisa kichwa chenu. Vema, basi tutawachukua nyote wawili. Vema.

¹⁴³ Huyu mama hapa, ulitikisa kichwa chako namna *hii*; aliyevaa nguo ya waridi. Kama Yesu Kristo anaweza kuniambia shida yako ni nini, ama jambo fulani kukuhusu wewe, je! utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake; ujue kwamba ni Yeye? Shida yako iko mgongoni mwako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Unaona? Unaona? Vema. Unaona? Unaona?

¹⁴⁴ Sasa, wewe, maskini Bibi hapo mwisho, hukulipata kwa sababu hali ya hewa ilikuwa ni mbaya. Una ugonjwa wa utumbo mpana. Ama moyo. . . Utumbo mpana, uko kwenye utumbo wako mpana.

Mwanamke huyu anayeketi karibu na wewe, ana ugonjwa wa moyo.

¹⁴⁵ Endapo hilo ni kweli, ninyi wanawake watatu inueni mikono yenu. Nami ni mgeni kwenu, mnaona.

Sasa je! mnaamini? Iweni na imani. Hivyo tu ndivyo mnavyopaswa kufanya.

¹⁴⁶ Maskini mama anayeketi papa hapa, akiniangalia moja kwa moja, sikujui mimi. Wewe ni mgeni kwangu. Huni—hunijui. Anayeketi moja kwa moja pale, akiwa na ninii ndogo nyeupe. . . . akiniangalia moja kwa moja. Naam, wewe. A-ha. Hunijui mimi. Bali unaugua, sivyo? Kwa namna fulani ulikuwa unahofu kidogo kuhusu jambo fulani. Ni uvimbe ulio kwenye ziwa lako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Sasa, unasema, “Uliona uvimbe.” Hakuna uvimbe unaonyesha.

¹⁴⁷ Hiyo ni kweli, hakuna uvimbe unaonyesha? Wala sikujui mimi. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba wewe ni nani? Hilo litakusaidia kidogo? Lingelisaidia kusanyiko hili? Sasa, kumbukeni, mwanamke huyu ameinua mkono wake juu. Weka mkono wako juu, sikujui mimi. Mungu anisaidie. Bibi Patterson. Hiyo ni kweli. Je! unaamini?

¹⁴⁸ Jambo lingine, huyo ni mama mkwe wako anayeketi karibu na wewe hapo. Je! unaamini? Anataka kuombewa. Amekuja kwa kusudi hilo. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia ana shida gani? Shida yake iko machoni mwake na masikioni mwake. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli.

Yeye yu hai! Yeye angali ni Mungu.

¹⁴⁹ Huyu hapa bibi anayeketi hapa nyuma, akiwa na kifafa. Yeye ana kifafa, na ana ugonjwa wa wanawake. Na jina lake ni Bibi Woods. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Simama kwa miguu yako kama hiyo ni kweli. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Ibilisi alikuacha hapo, dada. Mungu asifiwe! “Kama unaweza kuamini.” Amini tu.

¹⁵⁰ Huyu hapa mama anayeketi papa *hapa* nyuma. Ni mnyonge sana. Ni mgonjwa. Ndiyo kwanza atoke hospitalini. Ana—ana ugonjwa wa tumbo. Jina lake ni Bibi Kitchens. Simama, na uamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo amekuponya. Kamwe sijapata kumwona maishani mwangu.

¹⁵¹ Huyu hapa bibi aliye na ugonjwa wa kibofu nyongo. Je! unaamini kwa moyo wako wote, pia, ya kwamba Mungu atakuponya? Bibi Whittaker, je! unaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya? Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako, kama sisi hatufahamiani.

¹⁵² Je! Mnaamini Yeye yupo hapa? [Kusanyiko linashangilia na kusema, “Amina.”—Mh.] Ni kitu gani? Huyu ni shahidi mtetezi

wa Mungu. Haleluya! Enyi watu, aminini kwa moyo wenu wote! Huyu ni shahidi mtetezi wa Mungu.

153 Je! unamhukumuje? Je! unaamini ya kwamba Yeye ni wa kweli? Je! unaamini ya kwamba Neno Lake ni kweli? Yeye aliahidi! Juma zima, nimehubiri juu ya jambo hilo na kulionyesha katika Biblia, ya kwamba Yeye angefanya jambo hili katika siku hii. Je! unaamini ya kwamba ni Kweli? Je! unahukumu? Hukumu yako ni gani? Je! unaamini?

154 Hebu wale walio na kadi za maombi katika upande huu *hapa*, wasimame katikati ya marefu ya kanisa, *hapa*, walio na kadi za maombi, mstarini *hapa*; simameni katikati ya marefu ya kanisa, upande huu. Wale walio upande *ule*, walio na kadi za maombi, wasimame kwenye marefu *yale* ya kanisa, upande *huu*. Wale wanaoegemea upande *ule* mwingine, simameni kwenye marefu *haya*.

155 Wale walio huko juu, walio na kadi za maombi, shukeni mje mbele.

156 Wale walio kwenye mstari *huu* hapa, walio na kadi za maombi, simameni upande *ule*. Wale walio upande *huu* walio na kadi za maombi, simameni kwenye marefu *haya* ya kanisa *papa* hapa. Wale walio na kadi za maombi, *hapa*, simameni *hapa* kwenye marefu *haya*.

157 Sasa, simameni papo hapo sasa. Tutaenda upande huo mwingine katika kitambo kidogo. Pageni mstari wenu. Shukeni mje moja kwa moja. Mimi. . .

158 Sasa kaeni kimya, kwa kitambo kidogo tu, mahali mlipo. Simameni tu mahali mlipo, kwa kitambo kidogo tu.

159 Angalieni, ni wahudumu wangapi walio hapa ndani, wanaoamini, watu wacha Mungu kwelikweli wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ya kwamba agizo Lake la mwisho kwa Kanisa Lake, lilikuwa, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya”? Ni wangapi wenu ninyi wahudumu mnaoamini jambo hilo? Kama mnaamini, njeni hapa na msimame pamoja na mimi papa hapa tunapoomba. Ili kwamba watu hawa watakapoponywa, wataona haikuwa ni Ndugu Branham tu; ni ninyi, pia. Simameni moja kwa moja upande huu *hapa*, fanyeni mistari miwili papa hapa ambapo mstari utakapopitia. Loo, jamani! Mungu angeweza kufanya jambo gani tena? Sijui kitu. Angalieni wahudumu wakija kushuhudia jambo hili. Shukeni mwende moja kwa moja chini, pageni mstari wenu huku chini upande *huu*.

160 Ati? [Mtu fulani anamwambia Ndugu Branham, “Siwezi kuwafanya wasogee.”—Mh.] Ati? [“Hata siwezi kuwafanya wasogee hapa chini.”] Hiyo ni sawa. Ni vema. Tutawapata.

¹⁶¹ Sasa nitamwomba Ndugu Borders, meneja, aje hapa kwenye maikrofoni hii. Na ninataka apange mstari huu katika utaratibu, ili kwamba wapate kuja upande *huu*, warudi nyuma upande *ule*, kisha mrudi vitini mwenu, unaona, mtakapokuja.

Sasa wote wanaoweza kunisikia, inua mkono wako.

¹⁶² Angalia, hebu *hawa*, walio nyuma kabisa, waje kwanza; kisha waje wapite hivi, na wazunguke. Halafu muwape wengine nafasi. Wawazunguke wahudumu hawa hapa, mnapokwisha kuombewa, mwende moja kwa moja mrudi mkaketi kwenye viti vyenu. Halafu hebu naye Billy, atawaashiria mzunguke moja kwa moja na kuwaambia jinsi ya kuingia mstarini. Na kisha mara baada ya jambo hili kwisha, tutawaacha waondoke wapitie *kule*, kisha waje hivi.

¹⁶³ Sasa nyote, mnaofahamu, inua mkono wako sasa. Sawa, vizuri. Sasa Ndugu Borders atakuwa papa hapa kwenye maikrofoni, apate kushuhudia yale mnayopaswa kufanya. Vema.

¹⁶⁴ Sasa angalieni. Sababu ya mimi kufanya jambo hili, ni kwa sababu nawatakeni mfahamu. Siwajui ndugu hawa hapa. Ninajua wawili ama watatu wao. Huenda wakawa Methodisti, Baptisti, Presbiteri. Siwajui. Hakuna haja kwangu kusema jambo hilo. Mnaona? Sasa, nawatakeni mjue ya kwamba baada ya mimi kuondoka. . .

¹⁶⁵ Karibu wakati wote, wainjilisti huja mjini na kufanya kila kitu, mnaona, anawaombea wagonjwa na kila kitu. Unaona, hilo si sawa. Sitaki kuonyesha picha hiyo.

¹⁶⁶ Ninawatakeni mumwone Yesu. Juma hili, nimejaribu niwezavyo kabisa kuwaonyesha ya kwamba Yeye yupo hapa. Na kama mna imani, nyosheni mkono tu mumshike, si lazima kuingia mstarini. Lakini ukitaka kufuata Andiko hili, Uwepo Wake wa Kiungu, umegusa vazi Lake. Angalia tu, kile, watu hawa wakisimama hapa, muda mfupi uliopita, Mungu wa Mbinguni anajua sijapata kuwaona hao watu maishani mwangu. Nami ningeweza kuanzia papa hapa, katika dakika chache ningezimia. Ni wangapi wanajua ya kwamba Yesu, wakati jambo hilo lilipompata, yule mwanamke akitumia karama ya Mungu, alikuwa mnyonge? Ni wangapi wanaojua ya kwamba nguvu zilimtoka, zilikuwa ni uweza Wake? Nami ni mwenye dhambi. Lakini Yesu alisema, “Zaidi ya hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi ninaenda kwa Baba Yangu.”

¹⁶⁷ Sasa tutafanya maombi. Nami ninawataka wahudumu hawa wawe pamoja na mimi. Nitasimama moja kwa moja huku, pia, niweke mikono juu ya kila mmoja aliye mgonjwa. Na sasa kama mkininii. . .

¹⁶⁸ Kumbukeni! Sikilizeni! Sikieni Hilo! Aminini jambo hilo! Usipopitia hapa, ukiamini, “Hivi sasa limetatuliwa milele,” usije. Itakufanya tu uwe mgonjwa zaidi. Itazuia imani yako. Bali kama unaamini ya kwamba uko Mbele za Yesu Kristo,

wala si sisi watumishi Wake. Na sisi tunatekeleza tu, mashahidi, tunapoweka mikono yetu juu yenu, kwamba tunaamini hii kuwa ni Kweli. Na tunapowawekea mikono, aminini na mtoke hapa, mkifurahi, mkisema, “Asante, Bwana! Limetatuliwa.” Kamwe usibadilishe nia yako.

¹⁶⁹ Sasa kumbukeni. Hebu ninukuu jambo hili tena. Sikilizeni kwa makini. Moyo wako ndiyo baraza lako la wazee wa mahakama, juu ya kesi hii. Na matendo yako tokea hapa na kuendelea, yatakuwa, yatatamka kwamba hukumu yako ni nini. Ukija hapa ndani na kusema, “Vema, sijui,” unaona, unaona mahali ulipomhukumu. Yeye yuko mahakamani mbele ya kila mmoja wenu. Yeye yupo hapa, mbele zenu. Neno Lake liko hapa. Yeye huthibitisha Neno Lake. Uko hapa. Yeye, Yeye anashtakiwa na wewe, hashitakiwi na mimi. Mimi ninamwamini. Yeye anashtakiwa na wewe. Na kama unamwamini, na kama ukimwona ni mwaminifu kwa Neno Lake. . .

¹⁷⁰ Sasa wako karibu kuunyosha mstari huo, kwa hiyo wanafanya mstari hapa, unaona. Ninii tu, ninangojea tu mpaka atakapounyosha. Sogeeni kabisa na mfanye mstari mrefu. Na mrudi moja kwa moja nyuma jinsi mliyokuja, mtakapotoka.

¹⁷¹ Kama ulimwamini Yeye, basi jambo fulani litatukia. Kumbukeni, sasa, hakuna nguvu katika yeyote wa hawa wahudumu. Hakuna nguvu ndani yangu. Hakuna nguvu katika mtu yeyote, kuponya. Lakini tuna mamlaka kutoka kwa Mungu, kufanya jambo hili. Hatuna nguvu; tuna mamlaka. *Haya* hapa mamlaka yetu, Neno la Mungu, na Uwepo wa Yesu Kristo unathibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa. Nini? Mnapaswa kuponywa, kila mmoja.

¹⁷² Sasa hebu sote tufunge macho yetu tunapofanya maombi. Naye Ndugu Borders atakuwa amesimama hapa, akiongoza nyimbo na kuwaongoza watu. Mnapopitia hapa sasa, ombeni na mwamini.

¹⁷³ Ninyi nyote kusanyikeni, ndugu wahudumu. Mnaona ni kwa nini nimetenda jambo hili. Ili kwamba, nitakapoondoka, kusanyiko lenu linajua, pia, watu hawa wanaoponywa, ninyi ni watumishi wa Mungu, pia. Si mmoja tu. Mungu hana mtumishi mmoja tu; Yeye ana maelfu yao, wote watakaoamini jambo Hilo. Na tuinamishe vichwa vyetu. Mna haki tu ya kuwaombea wagonjwa, kama niliyo nayo mimi, Roberts, ama mtu mwingine yeyote yule.

¹⁷⁴ Baba wa Mbinguni, ninakushukuru tena, moyoni mwangu, na ninajua mioyo hapa. Una haki ya kuweka hili katika Neno, kwa kuwa tumeona likitenda kazi, na tunajua ya kwamba ni kweli. Na tunajua ya kwamba litatenda kazi kwa kila mtu. Nasi tunakuomba sasa, Bwana, tukiweka sawa nafsi yetu wenyewe, wakati tukijua Wewe upo hapa. Umejibu. Ulinena Neno Lako kwetu. Upo hapa.

¹⁷⁵ Sasa Wewe na ututie mafuta, Bwana, ili kwamba tutakapoweka mikono juu ya hawa wagonjwa, maskini watu wagonjwa wanaoketi hapa katika mvua hii alasiri ya leo, jalia kila mmoja wao apone, na aende nyumbani na awe mzima. Jalia wawe kama Ibrahimu, “kuyaita mambo ambayo hayakuwako, kama kwamba yalikuwako,” kwa maana Mungu alitoa ahadi. Nawe ndiwe uliyesema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hukusema kamwe wangepona papo hapo, bali ulisema wangepona. Nasi tunaamini jambo hilo, Bwana. Saidia kila—kila mtu aamini, Bwana, tunapoweka mkutano huu mkononi Mwako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunafuata Amri Zako. Amina.

¹⁷⁶ Sasa hebu mstari wa maombi na uanze, Ndugu Borders, chukua kadi ya maombi. [Ndugu Branham na wahudumu wanamwomba kila mtu aliye kwenye mstari wa maombi —Mh.]

¹⁷⁷ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...anayeamini? [Kusanyiko linashangilia na kusema, “Amina.”] Bwana awabariki.

¹⁷⁸ Sababu ya mimi kuunganisha mikono yangu pamoja na ninyi enyi ndugu wahudumu, hiyo ilikuwa ni kwa sababu baadhi yenu nyote mlikuwa mkiugua, pia, mnajua. Nanyi mkajiweka huku kuwaombea wengine, na kuachwa peke yenu. Si sawa. Ninaamini, tuliposhikana mikono, ninaamini ya kwamba Mungu aliheshimu jambo hilo.

¹⁷⁹ Na hapa, sasa, hawa—hawa hapa wale wasingeweza kwenda mkutanoni; sasa hebu na tuombe, kwa ajili ya lesi hizi.

¹⁸⁰ Baba wa Mbinguni, tumefundishwa, katika Biblia, ya kwamba—ya kwamba, “Walichukua kutoka katika mwili wa Mtakatifu Paulo, lesi na nguo.” Sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali Yesu. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utatuma baraka Zako pamoja na lesi hizi, na kuponya wote na kila mmoja wao. Wape afya, Bwana, kwa ajili ya utukufu Wako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba na kuwatuma. Amina.

¹⁸¹ Ninataka kusema jambo hili. Ya kwamba, nikipitia kwenye mstari, niliona wanawake na wanaume wakipakata watoto wachanga, nao walikuwa wamelowa maji. Hebu nikumbukeni tu, ndugu zangu wachungaji, ya kwamba, majuma kadhaa kutoka sasa, mtakuta kwamba, kulikuwako na jambo kubwa lililotukia hapa. Watapona. Ninasema ya kwamba asilimia tisini wao watapona. Hiyo ni kweli. Loo, mimi ilikuwa...Sijapata kuhisi imani ya aina hiyo. Ilikuwa ni ya ajabu sana. Ninaona ninyi mnaninii...Sasa tenda tu, nendeni tu na mfanye kama kwamba yote yamekwisha, haidhuru kama hukuhisi hivyo. Usininii...Kamwe Yeye hakusema, “Je! ulihisi?” Alisema, “Uliamini? Uliamini?” Na tunaamini. Naye yupo hapa sasa, nasi tunampa—tunampa sifa na utukufu, kwa yote ambayo amefanya.

¹⁸² Na enyi marafiki Wakristo wapendwa, ninajua watakuwa wakifunga mkutano huu katika dakika chache, nami ninataka kuwaambia jambo hili. Nisipokutana nanyi tena upande huu wa Mto, nitakutana nanyi Kule nikiwa na Injili ii hii, Jambo lili hili. Sasa kumbukeni tu, ya kwamba yale mliyokubali alasiri ya leo, moyo wako umekuwa ndiyo mzee wa mahakama. Umejiamulia, umetoa uamuzi.

¹⁸³ Sasa endeleeni kutenda. Sijali kama ulikuwa umelemaa wala usingeweza kusogea; bado endelea tu kuamini. Yeye, Yeye alisema, “Watapata afya! Watapata afya!” Hivyo ndivyo shahidi alivyosema, kila shahidi leo. Kote kote katika Biblia, Yeye... isipokuwa awe alisema jambo litatendeka lenyewe. Lakini katika jambo hili, “Watapata afya,” hivyo ndivyo ilivyo kuwekea mikono. Sasa kama ono lilitukia, na kusema, “jambo hili litatukia wakati fulani, wakati fulani,” ndipo anaweka wakati huo. Lakini katika suala hili hapa, Yeye alisema, “Watapata afya.” Amini hivyo, kwa moyo wako wote. Hebu tuimbe mara moja.

Hata twonane huko juu! Mungu.

Hata twonane Kwake kwema;

Hata twonane huko juu!

Mungu awe nanyi daima!

¹⁸⁴ Sasa kabla tu, hebu tupeane mikono na mtu fulani aliye karibu nawe, tuseme, “Mungu akubariki, rafiki Mkristo.” Msisogee. Kaeni tu, peaneni mikono pande zote. “Mungu akubariki, rafiki Mkristo.” Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu: Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, Roy.

¹⁸⁵ Sasa hebu na tumwinulie Kristo mikono, na kuimba

Hata twonane (hebu tufunge macho yetu na

tuinue mikono yetu sasa.) huko juu!

Hata twonane Kwake kwema!



KESI SWA64-0405

(A Trial)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 5 Aprili, 1964, katika Banda la Klabu cha 4-H, huko Louisville, Mississippi, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org